Miti iliyoanguka, Trees which fell.
- KI/VI: *Kitabu ulichonipa*, The book you gave me.
Vitabu ulivyonipa, The books you gave me.
- N: *Nyumba aliyojenga*, The house he built.
Nyumba alizojenga, The houses which he built.
- MA: *Tunda lililoiva*, The fruit which is ripe.
Matunda yaliyoiva, The fruits which are ripe.
Uso uliotakata, The face which is clean.
Nyuso zilizotakata, The faces which are clean.
- PA: *Pahali palipochafuka*. The place which is dirty.
- KU: *Kusoma kunakofaa*. Reading which is useful.

Briefly, from the above examples we get the following relative particles for all the noun classes:

MI/WA : *ye* and *o* KI/VI: *cho* and *vyo*

M/MI: *o* and *yo* N: *yo* and *zo*

MA: *lo* and *yo* U: *o* and *zo*

KU: *ko* PA : *po* and *zo*

The second way of rendering the relative pronouns is to attach the relative particles to the word *amba*, thus:

mtu ambaye... kitabu ambacho...

watu ambao... vitabu ambavyo...

mti ambao... nyumba ambayo...

miti ambayo... nyumba ambazo...

tunda ambalo... uso ambao...

matunda ambayo... nyuso ambazo...

kusoma ambako... pahali ambapo...

Originally Swahili relatives were expressed only by adding the relative particle to the verb. Adding the relative particle to the word *amba* to express relationship is a recent introduction into the Swahili language. It is, nevertheless, accepted as correct Swahili usage.

The relative of time is expressed by *-po-*, “when” e.g.

Alipokuja nilikuwa shuleni, “When he came I was at school.”

Ninaposoma sitaki kelele, “When I am reading I do not like noise”.

In the future tense, the relative particle *kapo* is used, e.g.

Utakapokuja... “When you come”.

Utakapokuja utakuta kazi tayari, “When you (will) come you will find the work ready”.

The relative of place is *ko*, “where”, e.g.

Sijui alikoweka kitabu kile, “I do not know where he put that book”.

Je, unajua alikokwenda? “Do you know where he went?”

Note that *mo* and *po* are also used instead of *ko* with some difference:

Usiingie chumbani walimo wageni. “Do not enter the room where the guests are”.

*Palipokaa/walipokaa wazee hakuna
cha kuogopa.* “Where old men are (sitting) there is nothing to
be afraid of”.

EXERCISE 32

Fill in the right relative particles:

1. Wali... kuwa watoto walipenda sana kucheza.
2. Miti ili... anguka jana ilikuwa mirefu sana.
3. Mwizi ali... iba shuleni amekamatwa na polisi.
4. Pahali tuna... kaa ni pazuri sana.
5. Nili... mwona sikumjua, nilifikiri ni mgeni.
6. Watoto wasikae mahali wali... kaa wazee, si vizuri.
7. Mwalimu wetu anapenda nyuso zili... takata.
8. Sijui ana.. weka vitabu vyake, njoo tutafute.

EXERCISE 33

Translate into Swahili:

1. The book which gave me is very nice.
2. Whose book is lost, mine or the teacher's?
3. The man who gave you that book is my father.
4. The house which you see was built by those people.
5. The name which you gave to your dog is not nice.
6. I like to see faces which are clean.
7. Our teacher does not like to see feet that are dirty.
8. The trees which they cut were not theirs.
9. Do not sit on a place which is not clean.
10. Do not eat fruits which are not ripe.
11. Do not read books that are bad, read good books.
12. I like reading which is useful.
13. The thief who stole our clothes is that one.
14. Come tomorrow, you will see the man you want.
15. Do not come tomorrow, you will not see the man you want.

EXERCISE 34

Study this conversation and then translate into English:

Tatu Hujambo, Amina?

Amina Sijambo, habari gani ?

Tatu Nzuri sana, habari za watoto?

Amina Nzuri tu. Unakwenda wapi?

Tatu Nakwenda shuleni kumwona mwalimu aliyekuja jana.

Amina Ndiyo, nimesikia kuna mwalimu aliyekuja jana.

Tatu Twende basi tukamwone, nasikia ni kijana sana.

Amina Nimesikia ni msichana aliyefaulu mwaka huu.

Tatu Watu waliotoka mbali wamekwisha fika shuleni kumpokea mwalimu mgeni.
Twende, bwana!

Amina Ngoja nivae viatu vyangu vile virefu.

Tatu Usikawie sana, sipendi kuwa mtu wa mwisho.

Amina Haya, twende dada, tupite njia hii ndiyo fupi.

LESSON 26

SWAHILI ADVERBS AND PREPOSITIONS

ADVERBS OF TIME

<i>juzi</i> , the day before yesterday	<i>sasa</i> , now
<i>jana</i> , yesterday	<i>kila siku</i> , every day
<i>kesho</i> , tomorrow	<i>sasa hivi</i> , just now
<i>keshokutwa</i> , the day after tomorrow	<i>siku zote</i> , always
<i>usiku</i> , at night	<i>bado</i> not yet
<i>mchana</i> , in daytime	<i>bado kidogo</i> , yet a little while
<i>asubuhi</i> , in the morning	<i>baadaye</i> , afterwards
<i>jioni</i> , in the evening	<i>kwanza</i> , at first
<i>zamani</i> , formerly	<i>mwishowe</i> , in the end
<i>zamani sana</i> , a long time ago	<i>mwanzoni</i> , in the beginning
<i>mapema</i> , early	<i>usiku wa manane</i> , in the dead of night

ADVERBS OF PLACE

<i>chini</i> , on the ground	e.g. <i>shuka chini</i> , come down
<i>juu</i> , above	<i>juu angani</i> , in the air
<i>mbele</i> , in front	<i>ruka, juu</i> , jump up
<i>nyuma</i> , behind	<i>yuko mbele</i> , he is in front
<i>mbele ya nyumba</i> , in front of the house	<i>yuko nyuma</i> , he is behind
<i>nyuma ya nyumba</i> , behind the house	
<i>mbele yangu</i> , in front of me	
So too with <i>-yako, yake</i> etc.	(refer Lesson Twenty)
<i>ndani</i> , inside	<i>wako ndani</i> , they are inside

<i>nje</i> , outside	<i>yuko nje</i> , he is outside
<i>katikati</i> , in the centre	<i>hapa ni katikati</i> , here is the centre/middle
<i>karibu</i> , near	<i>yuko karibu</i> , he is near
<i>mbali</i> , far away	<i>wako mbali sana</i> , they are far away
<i>hapa</i> ,	here
<i>hapahapa</i> ,	right here
<i>pale</i> ,	there
<i>palepale</i> ,	on the spot
<i>huko</i> ,	there
<i>huku na huko</i> ,	here and there
<i>popote</i> ,	everywhere/anywhere
<i>kokote</i> ,	everywhere/anywhere

ADVERBS OF MANNER

<i>bure</i> , in vain, gratis	<i>sawasawa</i> , evenly, O.K.
<i>hakika</i> , certainly	<i>mbalimbali</i> , different (ly)
<i>halisi</i> , that's it	<i>pamoja</i> , together
<i>hasa</i> , especially	<i>moja moja</i> , one by one
<i>hata kidogo</i> , not at all	<i>zaidi</i> , more
<i>ghafla</i> , suddenly	<i>tu</i> , only
<i>kabisa</i> , indeed	<i>hivi</i> , thus
<i>kamwe</i> , not, never	<i>hivyo</i> , in that way
<i>kidogo</i> , a little	<i>vilevile</i> , also
<i>labda</i> , perhaps	<i>pia</i> , also
<i>mno</i> , too much	<i>lakini</i> , but
<i>ovyo</i> , disorderly	<i>naam</i> , yes/ok
<i>polepole</i> , slowly	<i>ndiyo</i> , yes
<i>upesi</i> , quickly	<i>hapana</i> , no
<i>haraka</i> , quickly/fast	<i>siyo</i> , no

<i>vibaya</i> , badly	<i>vingine</i> , otherwise
<i>vizuri</i> , well	<i>vyovyote</i> , anyhow
<i>vigumu</i> , hardly	<i>kiume</i> , manly

NB Adverbs can also be formed by prefixing *ki* to nouns, thus: *kiungwana*, “like a gentleman” in the manner of a gentleman”.

Useful Expressions

<i>Fanya hivi</i> ,	Do (it) this way.
<i>Usifanye hivi</i> ,	Do not do (it) in this way.
<i>Sikusema hivi</i> ,	I did not say that.
<i>Hivyo ndivyo ulivyosema</i> ,	That is what you said.
<i>Fanya vyovyote upendavyo</i> ,	Do as you please wish.
<i>Mambo yako hivyo ulivyosikia</i> ,	Things as you have heard.
<i>Walisemaje ulipowauliza?</i>	What did they said when you asked them?
<i>Amekwendaje ?</i>	How did he go?
<i>Popote ulipo</i> ,	Where ever you may be.
<i>Kokote uendako nitakufuata</i> ,	I will follow you wherever you go.
<i>Huku na huko</i> ,	Here and there.
<i>Palepale</i> ,	On the spot.
<i>Hapa hapa</i> ,	Right here.
<i>Tazama alivyo</i> ,	Look at the way he is.
<i>Tazama nguo zilivyo chafu</i> ,	See how dirty the clothes are.
<i>Sikia simba anavyonguruma</i> ,	Hear how the lion is roaring.
<i>Hivi ndivyo mambo yalivyo</i> ,	That is the way things are.

EXERCISE 35

Insert the right affixes in the blank spaces:

1. Watu hawa ndivyo wali... sema.
2. Je, mmefanya ali... waambia?
3. Tazama mikono ya mtoto ili... michafu !
4. Je, unajua ali... kwenda?

5. Tuli... kuwa watoto tulicheza kila siku.

6. Kitabu kili... potea ni hiki hapa.

PREPOSITIONS

Some adverbs become prepositions when *ya* is added to them, e.g. *baada ya*, from *baada*; *ndani ya*, from *ndani* etc..., without changing the sense.

Examples:

Prep.:	<i>Njoo baada ya kula,</i>	Come after eating.
Adv. :	<i>Njoo baadaye,</i>	Come afterwards.
Prep. :	<i>Ingia ndani ya nyumba,</i>	Go inside the house.
Adv. :	<i>Ingia ndani,</i>	Go inside.
Prep.:	<i>Mbele ya shule,</i>	In front of the school.
Adv. :	<i>Njoo mbele,</i>	Come in front.
Prep. :	<i>Nyuma ya shule,</i>	Behind the school.
Adv. :	<i>Rudi nyuma,</i>	Go behind.
Prep.:	<i>Chini ya meza,</i>	Under the table.
Adv. :	<i>Kaa chini,</i>	Sit down.
Prep. :	<i>Nje ya nyumba,</i>	Outside the house.
Adv. :	<i>Usikae nje usiku,</i>	Do not stay outside at night.
Prep. :	<i>Katikati ya mji,</i>	In the centre of town.
Adv. :	<i>Kaa katikati,</i>	Sit in the middle.
Prep. :	<i>Kati ya shule na shamba,</i>	Between the school and the farm.
Adv. :	<i>Weka mpira kati,</i>	Put the ball in the centre.
Prep. :	<i>Kabla ya kula,</i>	Before eating.
Adv. :	<i>Amekula,</i>	He has eaten.
Prep. :	<i>Karibu na,</i>	Near to.
Adv. :	<i>Karibu atakuja,</i>	He is about to come.
Prep. :	<i>Mbali na shule,</i>	Far from the school.
Adv. :	<i>Ameenda mbali,</i>	He has gone far away.
Prep. :	<i>Zaidi ya moja,</i>	More than one.

Adv. :	<i>Mpe zaidi,</i>	Give him more.
Prep. :	<i>Miongoni mwa watu,</i>	Among the people.
Adv. :	<i>... no adv.</i>	
Prep. :	<i>Baina ya,...</i>	Between.....
Adv. :	<i>... no adv.</i>	
Prep. :	<i>Wako pamoja,</i>	They are together with them.
Adv. :	<i>Kaeni pamoja.</i>	Stay together.

LESSON 27

HOW TO TELL TIME IN SWAHILI

The Swahili day begins at 7 a.m. and ends at 6 p.m. It is called *siku* “day”. The night is also 12 hours beginning at 7 p.m. and ending at 6 a.m. From 6 a.m. to about 10 a.m. it is *asubuhi*, “morning”; from 11 a.m. to about 4 p.m. it is *mchana*, during the day; from 5 p.m. to about 8 p.m. it is *jioni*, “evening “. The night is *usiku*. which means also “at night”.

e.g. *Alikuja usiku*, “He came at night”. Likewise:

Alikuja mchana, “He came during the day”.

Alikuja asubuhi, “He came in the morning”.

Alikuja jioni, “He came in the evening “.

Swahili time can be reckoned from the English time system in the following manner:

1. From 7 am. to 12 noon: subtract 6 from the English time, and you get the corresponding Swahili time.

e.g. $7 - 6 = 1$: *saa moja*.

$8 - 6 = 2$: *saa mbili*.

$12 - 6 = 6$: *saa sita*. etc.

As the word *saa*, “hour” is in the N class, the words *moja*, *mbili*, *tatu*, etc. do not take nominal prefixes. We say: *saa tatu*, *saa nne*, *saa tano*, etc... Now let us see if you can tell time in Swahili. What time is it in Swahili when it is 9 p.m.? How do you get the Swahili equivalent of 9 p.m.? Of course, you subtract 6 from 9 and get 3; so it becomes *saa tatu usiku* in Swahili.

2. From 1 p.m. to 6 p.m. add 6 to get the Swahili time.

e.g. $1 \text{ p.m.} + 6 = 7$: *saa saba mchana*.

$3 \text{ p.m.} + 6 = 9$: *saa tisa mchana*.

$6 \text{ p.m.} + 6 = 12$: *saa kumi na mbili*.

3. Likewise, from 1 a.m. to 6 a.m. add 6 to get the Swahili time, thus:

$1 \text{ a.m.} + 6 = 7$: *saa saba usiku*.

$2 \text{ a.m.} + 6 = 8$: *saa nane usiku*.

$6 \text{ a.m.} + 6 = 12$: *saa kumi na mbili asubuhi*.

The expressions *kutwa*, “the whole day”, and *kucha*, “the whole night”, are common. e.g. *Tulifanya kazi kutwa*, “We worked the whole day”. So too, “*Hatukulala usiku kucha*, “We did not sleep the whole night”.

EXERCISE 36

Translate into English:

1. Je, ulikuja saa ngapi jana? Nilikuja saa moja jioni.
2. Ni saa ngapi?¹⁸ Sasa ni saa sita mchana.
3. Njoo kesho saa mbili asubuhi, nitakuwa nyumbani.

4. Je, unakwenda kazini saa ngapi? Saa moja na nusu.¹⁹
5. Je, shule inaanza saa ngapi? Inaanza saa moja.
6. Watoto lazima waende kulala saa moja jioni na waamke saa kumi na mbili asubuhi.
7. Je, siyo mapema mno (too early)? Ni vizuri, watapata afya (health).
8. Tulifanya kazi jana kutwa, tulichoka sana. Tulirudi nyumbani saa tatu usiku.
9. Je, uliamka saa ngapi leo? Niliamka saa kumi na moja.
10. Baba alichelewa kurudi, alikuja saa saba usiku.

¹⁸ *saa ngapi?* Literally means “how many hours”, i.e. “what time is it?”

¹⁹ *nusu* means “half”, so “half past seven” in this case.

LESSON 28

NOMINAL PREFIXES

SUMMARY

Noun Class	Adjective	Verb		Possessive	Of (-a)
		Aff.	Neg.		
M/WA	m/wa	a/wa	ha/hawa	w/w	w
M/MI	m/mi	u/i	hau/hai	w/y	w/y
KI/VI	ki/vi	ki/vi	haki/havi	ch/vy	chlvy
N	N	i/zi	hai/hazi	y/z	y/z
ØMA	Øma	li/ ya	hali/haya	l/ya	l/y
U	m/n	u/zi	hau/kazi	w/z	wiz
PA	pa	pa	hapa	p	P
KU	ku	ku	haku	kw	kw

VERB “TO BE IN A PLACE”

M/WA

yuko/wako (is, are)

MIMI

uko/iko

KI/VI

kiko/viko

N

iko/ziko

MA

liko/yako

U

uko/ziko

PA

pako

KU

kuko

U

uko/ziko

Singular

Plural

Mtoto yuko wapi?

Watoto wako wapi?

Mti uko hapa.

Miti iko hapa

Kitabu kiko mezani.

Vitabu viko mezani

Nyumba yako iko wapi?

Nyumba zako ziko wapi?

Yai liko jikoni.

Ufa uko wapi ?

Pahali pako wapi?

Kuimba kwake kuko wapi? Kuimba kwao kuko wapi? Kuimba kwao kuko wapi?

Mayai yako jikoni.

Nyufa ziko wapi?

Mahali penu pako wapi?

Kuimba kwao kuko wapi?

THIS AND THAT

M/WA huyu/hawa (this, these) yule/wale (that, these)

M/MI huu/hii ule/ile

KI/VI hiki/hivi kile/vile

N hii/hizi ile/zile

MA hili/haya ule/zile

PA hapa pale

KU huku kule

THAT AND THOSE (near you, or spoken about)

		Singular	Plural
M/WA	huyo/hao	mtu huo	watu hao...
M/MI	huo/hiyo	mti huo	miti hiyo...
KI/VI	huyo/hivyo	kitu hicho	vitu hivyo
N	hiyo/hizo	nyumba hiyo	nyumba hizo
MA	hilo/hayo	jina hilo	majina hayo
U	huo/hizo	uso huo	nyuso hizo
PA	hapo	pahali hapo	
KU	huko	kusoma huko	

VERBS: ORDERS AND WISHES

Singular	Plural	Singular	Negative Plural
<i>soma</i> ,	<i>someni</i> , read	usisome,	<i>msisome</i> , don't read
<i>njoo</i>	<i>njoooni</i> , come ²⁰	usije	<i>msije</i> , don't come
<i>kula</i>	<i>kuleni</i> , eat	usile	<i>msile</i> , don't eat
<i>nende</i>	<i>nendeni</i> , go	usiende	<i>msiende</i> , don't go
<i>nije</i>	<i>tuje</i> , may I come ²⁰	usije	<i>tusije</i> , may we not come ²⁰
<i>aje</i>	<i>waje</i> , he may come	wasije	<i>wasije</i> , they may not

[20](#) As already should this may be translated in various ways, e.g. *nije*, may mean “may I come? I should come, etc...” depend on the context. Practice alone will enable you to know the right word the right word to use in a given context.

PART TWO

LESSON 29 – 40

LESSON 29

TATU²¹ NA WATOTO WAKE NYUMBANI

Vocabulary

<i>nyumbani,</i>	at home
<i>shuleni,</i>	at school
<i>chakula bora,</i>	good, nourishing food
<i>yai, mayai</i>	egg, eggs
<i>maziwa,</i>	milk
<i>mboga,</i>	vegetable
<i>mchele, wali</i>	rice (cooking rice)
<i>matunda,</i>	fruits (sing. tunda, fruit)
<i>-bichi,</i>	unripe, uncooked
<i>-bivu,</i>	ripe
<i>kuiva,</i>	to be ripe, to be cooked
<i>safi,</i>	clean
<i>usafi,</i>	cleanliness
<i>chafu,</i>	dirty, dirty
<i>kukataza,</i>	to forbid
<i>karibu na,</i>	near, nearby
<i>mbali ni,</i>	far away from
<i>ugonjwa, magonjwa,</i>	sickness, diseases
<i>japo,</i>	although (also <i>ijapokuwa, ingawa, ingawaje</i>)

Tatu ni mama. Ana watoto waTatu Mashaka, Chausiku na Sijali. Tatu anakaa shamba pamoja na watoto wake. Ana shamba la matunda na mboga. Tatu anawapa watoto wake chakula bora kila siku: mboga, mayai, matunda, samaki, viazi, mchele/wali, maziwa, nyama, n.k.

Siku moja Tatu alimwona mtoto wake, Mashaka, akila matunda mabichi, akamkataza, kwa sababu si mazuri. Tatu alichukua tunda moja zuri akampa Mashaka. Mtoto huyo alifurahi sana, akasema, “Asante, mama.”

Siku nyingine Tatu alikwenda mjini pamoja na mtoto wake, Chausiku. Njiani Chausiku alipata kiu akataka kunywa maji ya mtoni. Mama yake alimkataza akisema, “Maji ya mtoni si safi kwa

kunywa, yana vidudu vya magonjwa mbalimbali. Ngoja tufike nyumbani nitakupa maji safi” Japo Chausiku alikuwa na kiu sana hakunywa maji yale, alingoja mpaka walipofika nyumbani. Tatu anawalea watoto wake vizuri; anawafundisha kwa maneno na kwa vitendo pia. Tatu ni mama mwema.

ZOEZI LA 37

1. Je, Tatu ana watoto wangapi? Taja majina yao.
2. Je, Tatu anakaa wapi? Anafanya nini?
3. Je, vyakula gani ni bora?
4. Je, nani alikula matunda mabichi ? Tatu alifanya nini ?
5. Je, mtoto alisema nini alipopewa tunda zuri na Tatu?
6. Je, kwa nini Tatu alimkataza Chausiku kunywa maji ya mto?
7. Je, Chausiku alifanya nini alipokatazwa kunywa maji ya mto na mama yake?
8. Je, Tatu ni mama mwema? Kwa nini unasema hivyo?
9. Je, Tatu alikwenda wapi na Chausiku?
10. Je, maji ya mto ni safi kwa kunywa? Kwa nini?

NYUMBANI : USEFUL EXPRESSIONS

<i>kutandika kitanda,</i>	to make a bed
<i>kupangusa meza,</i>	to dust a table
<i>kuandaa meza,</i>	to set a table
<i>fungua mlango, dirisha,</i>	open the door, the window
<i>funga mlango, dirisha,</i>	shut the door, the window
<i>kufua nguo chafu,</i>	to wash dirty clothes
<i>kupiga pasi nguo,</i>	to iron clothes
<i>kupiga deki,</i>	to wash the floor
<i>weka chakula mezani,</i>	put food on the table
<i>kuona njaa, kiu,</i>	to be hungry, thirsty
<i>kusafisha vyombo,</i>	to wash dishes

HADITHI

Vocabulary

chuma matunda, pick fruits

<i>jikoni,</i>	in the kitchen
<i>nyani,</i>	a baboon
<i>ogopa</i>	be frightened
<i>mayowe</i>	yells
<i>hodari</i>	brave
<i>fimbo</i>	stick

Tatu alikwenda shambani kuchuma matunda. Alipofika aliona mengine yameiva na mengine hayajaiva. Dada zake, Bahati na Amina, walitaka matunda. Walichuma matunda yote, mabivu na mabichi. Matunda mabichi waliyaweka jikoni yaive, matunda mabivu waliyala palepale. Walikuwa na njaa. Walipokuwa pale shambani alitokea nyani mmoja mkubwa. Tatu na dada zake waliogopa sana. Walikimbilia nyumbani wakilia, “Nyani, nyani! “Waliposikia mayowe hayo, Mashaka na dada zake, Chausiku na Sijali, walitoka nje. Mashaka alikuwa kijana hodari. Alichukua fimbo akaenda shambani kumfukuza nyani yule. Nyani yule alipomwona Mashaka anakuja na fimbo, akakimbia, akaingia porini.

ZOEZI LA 38

1. Je , nani alichuma matunda?
2. Je, matunda yote yalikuwa mabichi ?
3. Je, Tatu na dada zake waliogopa nini? Walifanya nini ?
4. Kwa nini Tatu na dada zake walikula matunda shambani?
5. Je , nani alimfukuza nyani?
6. Je, nyani alikwenda wapi?

AMINA NA MPISHI WAKE JIKONI

Vocabulary

<i>jiko, jikoni,</i>	kitchen, in the kitchen
<i>kijiko, vi-</i>	spoon(s)
<i>umma, nyuma</i>	fork(s)
<i>kisu, vi-</i>	knife, knives
<i>sufuria,</i>	metal cooking pot
<i>sahani,</i>	plate(s)
<i>kikombe, vi-</i>	cup(s)
<i>chai, sukari,kahawa,</i>	tea, coffee sugar

<i>siagi,jibini,</i>	butter, cheese
<i>mkate,</i>	bread
<i>asali,</i>	honey
<i>chumvi,</i>	salt

Amina Mpishi, leo unapika nini?

Mpishi Nitapika wali na samaki, najua wewe huli samaki, nitakupikia nyama.

Amina Vizuri sana, Je, wageni wote wanakula samaki, umewauliza?

Mpishi Hapana, sikuwauliza, ngoja nitakwenda kuwauliza sasa hivi.

Amina Fanya haraka, sasa ni saa tano, tunakula saa ngapi leo?

Mpishi Usiwe na wasiwasi chakula kitakuwa tayari mapema kama kawaida.

Amina Haya nenda, fanya kazi zako, ukitaka msaada niite, unasikia.

Mpishi Ndiyo mama.

CHUMBA CHA KULALA “THE BEDROOM”

Useful Expressions

<i>chumba, vyumba,</i>	room, rooms
<i>chumba cha kulala,</i>	bedroom
<i>kulala,</i>	to sleep, to lie down
<i>kuamka,</i>	to get up, wake up
<i>kuamsha,</i>	to awaken
<i>asubuhi,</i>	morning, in the morning
<i>jioni,</i>	evening, in the evening
<i>mchana,</i>	daytime, during the day
<i>mchana kutwa,</i>	the whole day
<i>usiku,</i>	night, at night
<i>usiku kucha,</i>	the whole night
<i>kitanda, vi-</i>	bed, beds
<i>kitandani,</i>	in the bed, on the bed
<i>mtu,mito,</i> pillow(s)	mtu, also means “river”)
<i>godoro, ma-</i>	mattress (es)

<i>taa, taa ya umeme,</i>	electric lamp
<i>kuwasha taa,</i>	to light a lamp
<i>kuzima taa,</i>	to put out light
<i>choo chooni.</i>	toilet, in toilet
<i>bafu. bafuni.</i>	bath-room, in the bath-room
<i>kuoga,</i>	to take a bath
<i>kunawa,</i>	to wash one's hands and face

[21](#) In these stories, Tatu appears without a husband; that should not worry you.

LESSON 30

TATU AENDA SOKONI

Vocabulary

<i>soko, sokoni</i>	market, in the market place
<i>mji, mjini,</i>	town, in the town
<i>njia, njiani,</i>	way, on the way
<i>hasi, mabasi,</i>	bus, buses
<i>basi, so,</i>	then, enough, stop
<i>kutuma, kutumwa</i>	to send, to be sent
<i>peke yangu, peke yako n.k. I alone, you alone, etc.</i>	I alone, you alone, etc.
<i>kupenda, kupendana,</i>	to love, to like, to love each other
<i>kukosa; kosa, makosa,</i>	to miss, to make mistake, a mistake, mistakes
<i>nafasi; wakati,</i>	opportunity, time
<i>kuongea,</i>	to talk, converse
<i>kusindikiza,</i>	to accompany, escort
<i>sababu; kwa sababu,</i>	cause, because

Tatu alipokuwa mtoto alikuwa na rafiki jina lake Chenga. Tatu na Chenga walipendana sana. Kila siku walikwenda shuleni pamoja, walicheza pamoja. Siku moja Tatu alitumwa na mama yake sokoni. Njiani alikutana na Chenga, wakaamkiana hivi:

Chenga: Jambo (hujambo) Tatu?

Tatu: Sijambo, je, wewe hujambo?

Chenga: Mimi sijambo kabisa, wewe je?

Tatu: Usiwe na shaka, mimi ni mzima tu.

Chenga: Ni furaha kubwa leo kukutana nawe peke yako saa hizi. Unakwenda wapi?

Tatu: Ninakwenda sokoni, mama amenituma peke yangu leo.

Chenga: Je, nikusindikize? Sina kazi, nitafurahi kwenda nawe.

Tatu: Ukitaka twende, Naogopa kwenda peke yangu.

Chenga: Ni bahati kwangu kupata nafasi hii.

- Tatu:** Bahati gani? Mbona tunaonana kila siku?
- Chenga:** Ndiyo, lakini leo ni tofauti na siku nyingine.
- Tatu:** Tofauti gani? Mimi naona sawa tu kama jana na juzi na siku zote.
- Chenga:** Iko tofauti , nitakwambia sasa hivi. Twende tu.
- Tatu:** Haya, niambie basi, kitu gani hicho? Siri, au nini?
- Chenga:** Usiwe na haraka, nitakwambia tu, ngoja kidogo.
- Tatu:** Ningoje nini? Niambie tu, niko hapa, sitakukimbia.
- Chenga:** Nilitaka kukwambia tangu siku nyingi , lakini sikuwa na nafasi.
- Tatu:** Mbona unazidi kuzunguka tu wala husemi chochote cha maana.
- Chenga:** Ni hivi, ningependa wewe na mini, tukisha kuwa wakubwa tuoane, unasemaje? Hupendi kuwa mke wangu wa maisha?
- Tatu:** Maneno yako hayana maana, kama umekosa la kusema heri kunyamaza.
- Chenga:** Najua huwezi kukubali mara moja, nenda ukafikiri polepole.
- Tatu:** Sina cha kufikiri, inafaa tuongee mambo mengine.
Unaona basi lile?
- Chenga:** Twende upesi, tutachelewa, mabasi hapa ni shida sana siku hizi.

ZOEZI LA 39

1. Tatu alikutana na nani alipokwenda sokoni?
2. Nani alisema, “Tofauti gani ?”
3. Nani alisema, “Kitu gani hicho?”
4. Nani alimsindikiza Tatu?
5. Nani alisema, “Maneno yako hayana maana?”
6. Nani alisema, “Inafaa tuongee mambo mengine?”
7. Nani alisema, “Ni bahati yangu?”
8. Chenga alimwambia nini Tatu kuhusu kuoana?
9. Je, mabasi ni rahisi au ni shida kuyapata?
10. Je, Tatu alikuwa mtoto au mtu mzima wakati huo?

USEFUL EXPRESSIONS

Bei gani?

What is the price?

<i>Machungwa haya ni thumni kila,</i>	These oranges are fifty cents each
<i>moja na yale pale ni senti thelathini,</i>	and those there are thirty cents each
<i>Nipe matano ya thumni,</i>	Give me five for fifty cents each
<i>Ndizi, je, bei gani?</i>	What is the price of the bananas?
<i>Ndizi ni nne shilingi,</i>	Bananas are four for a shilling
<i>Mbona ghali hivi?</i>	Why are they so dear?
<i>Ndiyo bei yake situ hizi,</i>	This is the price nowadays.
<i>Ebu, nipe nyanya mbili,</i>	Please give two tomatoes
<i>Ni bei gani jumla?</i>	What is the total price?
<i>Nipe shilingi kumi,</i>	Give me ten shillings
<i>Tatu, bado unanunua?</i>	Tatu, are you still buying?
<i>Nimemaliza, twende,</i>	I am ready, lets go.
<i>Vitu vimepanda bei!</i>	Things have become so expensive!
<i>Ndugu yangu, sijui tutafanya nini sasa ?</i>	Oh dear, I don't know what we should do now?
<i>Sisi watu wadogo tuna taabu, kweli</i>	We people of low income are in trouble, indeed!
<i>Basi lile, linakuja,</i>	There comes the bus.
<i>Kwa heri, dada,</i>	Bye bye, dear sister

LESSON 31

DUKANI

Vocabulary

<i>duka ma-</i> ,	shop, shops
<i>madukani</i> ,	at the shopping centre
<i>kwenda dukani</i> ,	to go shopping, to go to the shop
<i>kuuza; kununua</i> ,	to sell, to buy
<i>nguo</i> ,	clothes, cloth, dress, dresses
<i>nguo mpya nguo</i>	new close, old dress
<i>ya zamani</i> ,	
<i>kushona; cherehani</i> ,	to sew, sewing machine
<i>kupima nguo</i> ,	to take measure of a dress
<i>nipime nguo</i> ,	take my measure of a dress
<i>mashono bei gani?</i>	how much do you charge for sewing?
<i>inategemea kitambaa</i>	it all depends on the material
<i>suruali, koti</i> ,	a pair of trousers; a coat
<i>blauzi; sketi</i>	blouse, skirt
<i>sweta; chupi, vesti</i> ,	sweater, underpants, vest
<i>taulo; shuka; mashuka</i> ,	towel; bedsheet; bedsheets
<i>blanketi; nguo za watoto</i> ,	blanket(s); children's clothes
<i>binzari; pilipili</i> ,	curry powder; pepper

Tatu aliwaambia watoto wake waende dukani kununua vitu. Chausiku alisema, “Mama nitakwenda peke yangu dukani siogopi kitu”. Mashaka aliposikia vile alifurahi kwa sababu hakutaka kwenda dukani ; alitaka kucheza mpira. Basi , Chausiku aliondoka mara moja. Alifika dukani akakuta watu wengi. Aliuliza, “Je, mchele uko?” Mwenye duka alijibu,” Mchele uko, dada; unataka kiasi gani?” Chausiku alijibu, “Nipe kilo tano. Nipe pia nusu kilo ya binzari, robo kilo ya pilipili na kilo moja viazi. Nipe upesi nikimbie nyumbani, mama ananingojea njiani kwa sababu usiku umeingia nami niko peke yangu.”Mwenye duka alisema, “Haya, dada Chausiku, vitu vyako hivi hapa, nipe shilingi kumi na thumni. Chausiku alisema, “Sina shilingi kumi na thumni”, ninazo shilingi tisa na thumni tu. “Mwenye duka alisema, “Haya, si kitu, nipe hizohizo tu. “Chausiku alitoa fedha, akachukua vitu vyake, akaondoka mbio. Alifika nyumbani

kabla giza halijazidi.

ZOEZI LA 40

1. Tatu aliwaambia nini watoto wake?
2. Nani alikwenda dukani?
3. Kwa nini Mashaka hakutaka kwenda dukani?
4. Chausiku alinunua nini na nini dukani?
5. Mwenye duka alitaka shilingi ngapi? Alipata shilingi ngapi?
6. Je, Chausiku alinunua binzari kilo ngapi?
7. Je, nani alisema, “Lete hizohizo tu?”
8. Je, Chausiku alifika nyumbani lini?
9. Je, Chausiku alikwenda dukani na nani?
10. Je, Chausiku aliogopa kwenda peke yake?

Useful Expressions

<i>Dukani; madukani,</i>	In, at the shop(s); shopping centre.
<i>Bei; bei gani?</i>	Price; what is the price?
<i>Viatu vimepanda bei,</i>	Prices have gone up.
<i>Punguza bei,</i>	Reduce the price
<i>Ongeza bei, pandisha bei,</i>	Increase the price.
<i>Ndizi hizi bei gani?</i>	What is the price of these bananas?
<i>Samati hizi bei gani?</i>	How much are these fishes?
<i>Samaki mmoja ni shilingi mbili.</i>	They are two shillings each.
<i>Mbona ghali sana?</i>	Why are they so expensive?
<i>Si ghali, ndiyo bei yao,</i>	They are not expensive, that’s the price.
<i>Haya, nipe mbili,</i>	Well, give me two.
<i>Usiuze ghali namna hii.</i>	Don’t sell at such a high price.
<i>Nisipofanya hivyo sipati faida</i>	If I don’t do that I will get no profit.

LESSON 32

BARABARANI

Vocabulary

<i>mume (wa),</i>	husband, (her)
<i>lami,</i>	tarmac
<i>dereva,</i>	driver
<i>barabara, barabarani,</i>	road, on the road
<i>gari; magari,</i>	car, cars
<i>kuendesha,</i>	to drive
<i>kusimama; kusimamisha,</i>	to stop, to make stop
<i>kukimbiza gari.</i>	drive fast
<i>tope, matope</i>	mud
<i>utelezi, kuteleza,</i>	slippery, to slip
<i>mvua,</i>	rain, to rain
<i>kukwama, kusukuma,</i>	to get stuck, to push
<i>kupanda, kushuka,</i>	to climb up, to descend
<i>kwenda kwa gari,</i>	to go by car

Amina, dada yake Tatu, anafahamu kuendesha gari. Mumewe ana gari jipya aina ya VW. Amina ni dereva hodari, haendeshi mbio, anajua kuwa kukimbiza gari ni hatari. Ukienda kwa gari lake utafurahi, hutaogopa.

Siku moja, Amina alikwenda shambani kwa gari. Njiani aliuliza habari za barabara, kwa sababu mvua ilinyesha usiku. Madereva wengine walimwambia njia ilikuwa mbaya sana, yenye matope mengi na utelezi.

Basi, Amina aliendesha polepole sana, Alikutana na lori moja. Dereva wa lori alikuwa akiendesha mbio. Amina alikwenda pembeni kumpisha, na hapo alikwama vibaya sana. Kwa bahati lori lile lilikuwa na watu wengi wenye nguvu. Walisaidia kusukuma gari la Amina. Alipotoka katika matope, Amina alifurahi sana. Alisema, “Asanteni sana, ndugu. Sijui ningefanya nini peke yangu.” Watu wale walimsifu Amina kwa uhodari wake. Walisema, “Dada, wewe ni dereva hodari, lakini barabara hizi hazina dereva hodari, kila dereva hukwama mara kwa mara. Kukwama ni desturi katika barabara zetu kwa sababu hakuna/hazina lami.

ZOEZI LA 41

1. Je, kwa nini Amina alikwama?
2. Je, nani alimsaidia kusukuma gari lake?
3. Je, kwa nini ni desturi kukwama katika barabara zetu?
4. Je, nani alikwenda mbio?
5. Je, nani ni dereva hodari? Amina au dereva wa lori?
6. Je, Amina huendesha mbio? Kwa nini?
7. Je, kwa nini Amina aliuliza habari za barabara?
8. Je, Amina alipata habari gani za barabara?

Useful Expressions

<i>Petroli, stesheni ya petrol,</i>	petrol, petrol station
<i>nipe petroli lita kumni,</i>	give me 10 litres of petrol
<i>hebu, angalia oili,</i>	check the oil
<i>pima upepo,</i>	check the pressure (of tyres)
<i>jaza upepo,</i>	fill in the tyres
<i>kuna pancha,</i>	there is a puncture
<i>ziba pancha hii,</i>	fill this puncture
<i>hakuna pancha; valvu inavuja,</i>	no puncture, valve leakage
<i>gari limeharibika,</i>	the car is out of order
<i>tengeneza gari,</i>	repair a car
<i>kuegesha gari,</i>	to park a car
<i>pita kushoto, kulia,</i>	keep left, right
<i>njia ina matope sana,</i>	the way is very muddy
<i>nenda polepole,</i>	go slowly
<i>weka cheni, vingine hupiti,</i>	put chains; otherwise you won't pass
<i>ni hatari; kuna hatari,</i>	it is dangerous; there is danger
<i>gari haliwaki; limewaka,</i>	car does not start; it has started
<i>washa gari; zima gari,</i>	start the car; switch off

LESSON 33

TATU BAHARINI

Vocabulary

<i>bahari, baharini,</i>	ocean; in the ocean
<i>kuogelea,</i> <i>kupiga mbizi,</i>	to swim; to dive
<i>kuvua samaki,</i>	to fish
<i>kuzama,</i> <i>kuzamisha,</i>	to sink; to cause to sink
<i>kuelea, meli,</i>	to float; ship
<i>baharia,</i> <i>mwanamaji,</i>	a sailor, seaman
<i>haramia,</i> <i>maharamia,</i>	sea pirate(s)
<i>kuchafuka,</i>	to be angry, e.g. <i>bahari imechafuka</i> , “the sea is rough” <i>Baba amechafuka leo</i> , “father is angry today.”
<i>katika bahari,</i>	in the sea, in the ocean
<i>katikati ya bahari,</i>	in the middle of the ocean
<i>licha,</i>	let alone, not to mention

Siku moja Tatu alikwenda baharini kuogelea. Alikwenda pamoja na watoto wake. Ilikuwa ni mara ya kwanza kwa watoto wake kufika baharini, licha ya kuogelea. Sijali aliogopa kuingia majini, hasa alipoona mawimbi yakipanda na kushuka kwa nguvu. Mashaka alijitupa majini akajaribu kuogelea. Mama yao alimshika Sijali mkono akamchukua polepole mpaka kweye maji mengi. Chausiku na Mashaka walimfuata mama yao nyuma. Tatu aliwaonyesha namna ya kuogelea. Baada ya muda mfupi Tatu na watoto wake walianza kucheza majini bila woga. Walipochoka kuogelea, Tatu na watoto wake walikwenda kuangalia meli. Siku hiyo, meli nyingi zilifika kutoka nchi mbalimbali zenye kufanya biashara na nchi hii. Meli hizi zilileta bidhaa na kuchukua mazao ya nchi hii kupeleka nchi za nje. Watoto walimwuliza Tatu maswali mengi kuhusu meli na safari zake. Tatu alijibu maswali machache na hapo aliwaambia watoto wake, “Twendeni nyumbani sasa, nitajibu maswali yenu tukifika nyumbani.”

ZOEZI LA 42

1. Je, Tatu alikwenda wapi na watoto wake?
2. Je, nani aliogopa kuingia baharini ?
3. Je, Mashaka aliogopa kuingia majini?
4. Je, nani alijaribu kuogelea?
5. Je, Chausiku alifanya nini baharini ?
6. Je, Tatu alipochoka kuogelea alifanya nini ?
7. Je, meli zinakuja kufanya nini?
8. Je, nani aliuliza maswali mengi?
9. Je, Tatu alijibu maswali yote ya watoto wake?
10. Je, nani alishikwa mkono baharini ?

Useful Expressions

<i>maji kupwa; maji kujaa,</i>	low tide; high tide
<i>maji ya chumvi; maji matamu,</i>	salt water; sweet water (not salty)
<i>mvuvi wa samaki, wa-,</i>	fisherman. -men,
<i>kusafiri majini,</i>	to sail
<i>bandari, bandarini,</i>	port; at the port
<i>kutia nanga, nanga.</i>	to lower the anchor; anchor
<i>kung'oa nanga.</i>	to depart (of ship)
<i>homa ya baharini.</i>	sea sickness
<i>meli imezama,</i>	the ship has sunk
<i>wimbi; mawimbi,</i>	wave, waves
<i>je, unajua kuogelea?</i>	can you how to swim?
<i>sijui hata kidogo,</i>	I can't swim at all
<i>nitakufunza kuogelea,</i>	I will teach you how to swim
<i>kuogelea ni mchezo mzuri,</i>	swimming is a very good game
<i>si vigumu kuogelea,</i>	it is not difficult to swim,
<i>unaelea tu,</i>	you just float
<i>jaribu kuogelea hapa,</i>	try to swim here, the water
<i>maji si mengi</i>	is not deep

LESSON 34

TATU SERENGETI

Vocabulary

<i>nyama, nyama mbichi,</i>	meat, raw meat
<i>mnyama, wanyama,</i>	animal, animals
<i>mnyama wa porini, wa-,</i>	wild animals
<i>mbuga ya wanyama,</i>	plain reserved for animal
<i>bustani ya wanyama</i>	zoo
<i>simba,</i>	lion
<i>tembo,</i>	elephant
<i>chui,</i>	leopard
<i>pundamilia,</i>	zebra
<i>fisi,</i>	hyena
<i>swala,</i>	impala
<i>sungura,</i>	hare
<i>kifaru,</i>	rhinoceros
<i>kiboko,</i>	hippo(s)
<i>nyati,</i>	buffalo
<i>nyani,</i>	monkey(s)
<i>nguruwe,</i>	pig
<i>nguruwe mwitu,</i>	wild pig
<i>Mbuni,</i>	ostrich
<i>twiga,</i>	giraffe

Wanyama wa nyumbani Domestic animals

<i>mbwa,</i>	dog
<i>paka,</i>	cat
<i>mbuzi,</i>	goat
<i>kondoo,</i>	sheep

<i>ng'ombe,</i>	cow, cattle
<i>kuku,</i>	chicken
<i>punda,</i>	donkey
<i>farasi,</i>	horse

Tanzania kuna mbuga kubwa ya wanyama wa porini. Je, unajua jina la mbuga hiyo! Inaitwa Serengeti. Iko karibu na mji wa Arusha. Serengeti kuna wanyama wa kila aina, wakubwa na wadogo, kwa mfano: tembo, twiga, kifaruru, simba, chui, nyati, mbuni, swala, na wengine wengi. Ukitaka kuwaona wanyama wote hawa nenda Serengeti. Kila mwaka watu wengi huja Serengeti kuona wanyama. Wanatoka nchi mbalimbali: Ulaya, Marekani, Asia, na nchi nyingine. Tatu na watoto wake walisikia habari za Serengeti. Siku moja, walikwenda kuona wanyama Serengeti. Walipofika Arusha, walikutana na watalii wengi, wakaenda Serengeti pamoja. Tatu alifurahi sana kupata nafasi hii kuwaonyesha watoto wake mbuga hii kubwa ya wanyama. Japo walikuwa ndani ya gari, Sijali aliogopa sana alipoona simba amelala na twiga wakila majani. Mama yake alimwambia, “Usiogope, hakuna hatari.” Mashaka na Chausiku waliongea peke yao, sijui waliongea nini. Nafikiri waliongea juu ya wanyama wa porini. Hii ilikuwa mara yao ya kwanza kuona wanyama wengi namna hii. Walifurahi sana. Jioni, Tatu na watoto wake walirudi Arusha mjini, wakalala kwa shangazi yao. Watoto wake walieleza mambo waliyoyaona Serengeti. Shangazi yao alifurahi kusikia hadithi zao, mwishowe alisema, “Mimi pia nitakwenda Serengeti mwaka ujao mtakapokwenda, au mnasemaje? Watoto walijibu wote pamoja, “Ndiyo, shangazi, twende pamoja; Serengeti ni kuzuri sana. Ni moja ya maajabu ya dunia, au sivyo mama?” Mama yao alikuwa bafuni; hakisikia walichosema watoto wake. Kama angesikia, bila shaka angekubaliana na watoto wake.

ZOEZI LA 43

1. Je, Serengeti ni nini? Iko wapi?
2. Je, watu hufika Serengeti kufanya nini?
3. Je, nani aliogopa simba Serengeti?
4. Je, watalii wanaokuja Serengeti hutoka nchi gani?
5. Je, Tatu alikutana na watalii wapi?
6. Je, nani alisema, “Hakuna hatari?” Kwa nini alisema hivyo?
7. Je, Tatu na watoto wake walilala wapi walipotoka Serengeti?
8. Je, shangazi yao alisema nini?
9. Je, nani alisema Serengeti ni moja ya maajabu ya dunia?
10. Je, nani alikuwa bafuni?

USEFUL EXPRESSIONS

Je, umepata kuona simba?

Have you ever seen a lion?

<i>Je, umekwishafika Serengeti?</i>	Have you been to Serengeti?
<i>Bado sijaona simba, wewe je?</i>	I have not yet seen a lion, how about you?
<i>Twende Serengeti</i>	Let us go to Serengeti to
<i>tukaone simba,</i>	see lions.
<i>Twende Ofisi ya utalii Arusha,</i>	Lets us go to the tourist office in Arusha.
<i>Je, unapenda kuwinda?</i>	Do you like hunting?
<i>Sijui kupiga bunduki,</i>	I don't know how to shoot a gun.
<i>Sipendi kuwinda, ni hatari,</i>	I don't like hunting, it is dangerous.
<i>Ndugu yangu ni mwindaji hodari,</i>	My brother is a good hunter.
<i>Ana shabaha sana,</i>	He/she has a good shot.
<i>Ana leseni ya kuwinda tembo,</i>	He has a permit to hunt elephant.
<i>Siku moja alifukuzwa na</i>	One day he was chased by
<i>tembo lakini haachi kuwinda,</i>	elephant. but he did not stop hunting.
<i>Siku moja alikutana na simba</i>	One day he met a lion face
<i>porini ana kwa ana hakujua</i>	toface, he did not know how
<i>bunduki yake ilivyoanguka,</i>	his gun dropped (from his hand)
<i>Kuwinda kunapunguza,</i>	Hunting reduces the number
<i>wanyama, ijapokuwa</i>	of animals, even though they
<i>wanazaliana</i>	reproduce themselves
<i>Zamani dunia iijaa</i>	Formerly the earth was full
<i>wanyama,</i>	of animals
<i>lakini leo wamebaki wachache tu</i>	But today only a few remain
<i>Nyama ya nguruwe</i>	Meat from wild pigs is good,
<i>mwitu ni nzuri, lakini</i>	but the meat from impala is
<i>nyama ya swala ni nzuri zaidi.</i>	better

LESSON 35

BARS AND RESTAURANTS

Useful Expressions

Some people like to take some refreshments after visiting places like Serengeti, so here are some of the expressions you may need:

<i>chai; chai ya rangi</i>	tea, tea without milk
<i>kahawa; kahawa ya rangi</i>	coffee, coffee without milk
<i>maji ya machungwa,</i>	orange squash, orange juice
<i>maziwa moto; baridi,</i>	hot milk, cold
<i>bia moja baridi sana,</i>	one very cold beer
<i>bia moja moto,</i>	one warm beer
<i>soda na barafu,</i>	soda with ice
<i>Leo kuna chakula gani?</i>	What kind of food is there today?
<i>Leo kuna viazi, nyama</i>	Today, there are potatoes, meat
<i>na matunda,</i>	and fruit
<i>Je, kuna sikilimu?</i>	Is there ice cream?
<i>Je, naweza kupata saladi?</i>	Can I get some salads?
<i>Bila shaka bwana, utapata,</i>	Certainly sir, you will get it
<i>Niletee maji baridi na wiski,</i>	Bring me cold water and whisky.
<i>Wiski pegi ngapi?</i>	How many pegs of whisky (do you want?)
<i>Nipe nusu glasi,</i>	Give me half a glass, how many
<i>ni pegi ngapi?</i>	pegs is it?
<i>Ebu, niletee karoti kidogo,</i>	Bring me some carrots.
<i>nyama ya kondoo,</i>	mutton
<i>nyama ya ng'ombe,</i>	beef
<i>nyama ya nguruwe,</i>	pork
<i>nyama ya kuku,</i>	chicken
	Do you have roast meat here?

Je, kuna nyama ya kuchoma hapa?

Ndiyo, iko, unataka

kiasi gani?

Je, wanaweka vitunguu

na pilipili?

Ndiyo, kama unataka

watakuwekea,

Je, unakunywa nini?

Nakunywa “ndovu”²² baridi,

Yes, we have, how much do
you want?

Do they put in onions
and pepper?

Yes, if you so desire they will
put them in.

What do you drink?

I drink cold ndovu.

²² *Ndovu*: a brand of beer brewed in Tanzania. Other brands are: *Safari, Plisner, Kilimanjaro, Castle, Kibo, Guinness, Serengeti*, etc.

LESSON 36

KIWANJA CHA NDEGE

Vocabulary

<i>kiwanja; kiwanja cha ndege,</i>	plot, ground, airport
<i>ndege; kwenda kwa ndege,</i>	bird, aircraft, plane, to go by air
<i>kuruka kwa ndege,</i>	to fly (by aircraft)
<i>kushuka; kutua,</i>	to descend, to land
<i>kusafiri kwa ndege,</i>	to travel by air
<i>kupima mizigo,</i>	to check
<i>mzigo; mizigo,</i>	load, loads, luggage
<i>sanduku; masanduku,</i>	suitcase(s)
<i>juu ; juu angani,</i>	up, up in the sky
<i>anga; angani,</i>	sky, in the sky
<i>rubani, ma-,</i>	pilot(s)
<i>wafanyakazi wa ndege,</i>	crew
<i>kwenye kiwanja cha ndege,</i>	at the airport
<i>kukaguliwa na polisi,</i>	to be checked by the police
<i>kuteka nyara ndege,</i>	to hijack plane

Tatu alikuwa na rafiki, jina lake Wambura. Siku moja Wambura alimwandikia Tatu barua. Katika barua ile alisema, “Salamu, rafiki yangu, nitakuja kwa ndege keshokutwa, tutaonana na kuongea mengi...” Tatu alikwenda kiwanjani kumpokea rafiki yake. Wambura alitoka Nairobi kwa ndege ya asubuhi, waliondoka Nairobi saa mbili na walifika Arusha saa mbili na nusu. Ndege ilipotua, Wambura alitoka pamoja na wasafiri wengine. Tatu alimpokea mizigo yake na kuiweka katika tekisi. Njiani waliongea kwa furaha, mara kwa mara walicheka sana. Dereva wa tekisi alifurahi pia kusikiliza mazungumzo yao. Kwa kweli ni furaha kuona watu wanaopendana.

Walipofika nyumbani kwa Tatu, watoto walikuja kumsalimu mgeni. Mashaka alisaidia kuchukua mizigo na Chausiku aliandaa meza. Sijali alikuwa nje akicheza na wenzake. Mama yake alimwita, akaja mara moja. Jioni Wambura aliwasimulia habari za safari yake ya ndege.

ZOEZI LA 44

1. Je, rafiki ya Tatu ni nani? Anakaa wapi?
2. Je, barua ilitoka kwa nani? Ilisema nini?
3. Je, rafiki ya Tatu alifika Arusha saa ngapi?
4. Ndege ilichukua muda gani kutoka Nairobi mpaka Arusha?
5. Je, kwa nini dereva wa tekisi alifurahi?
6. Je, Sijali alikuwa wapi mama yake alipomwita?
7. Je, nani alisaidia kuchukua mizigo?
8. Je, Chausiku alifanya nini?
9. Je, nani alisafiri kwa ndege na baadaye kusimulia juu ya safari yake?
10. Je, ndege ilipotua Wambura alifanya nini?

Useful Expressions

<i>barua ya ndege,</i>	airmail.
<i>kupeleka barua kwa ndege,</i>	To send letters by airmail.
<i>kuondoka; ndege imeondoka,</i>	To depart, the aircraft has taken off
<i>kupokea mgeni,</i>	to receive a guest.
<i>mgeni alipokelewa vizuri sana,</i>	The guest was very well received.
<i>kusindikiza mgeni,</i>	To see a guest off, to escort.
<i>kuaga; kuagana.</i>	To take leave off, to part company.
<i>ndege kuanguka,</i>	Air crash.
<i>ajali ya ndege,</i>	Air accident.
<i>Barua ya ndege</i>	Airmail takes one hour
<i>inachukua saa moja</i>	from Arusha
<i>toka Arusha mpaka Nairobi,</i>	to Nairobi.
<i>kufunga mkanda;</i>	To tie the belt, to untie
<i>kufungua mkanda,</i>	the belt.
<i>kuvuta sigareti,</i>	to smoke.
<i>Msivute mpaka</i>	Don't smoke until we are up
<i>tufike angani</i>	in the air.
<i>Zimeni sigara zenu sasa,</i>	Put off your cigarrattes now.
<i>Mnaweza kuvuta sasa,</i>	You may smoke now.
<i>Kaeni wima vitini,</i>	Stay up right in your chairs.

<i>Mnaweza kulala sasa,</i>	You may recline now.
<i>Je, hupendi safari ya ndege?</i>	Don't you like to go by air?
<i>Ninaogopa kusafiri angani,</i>	I am afraid to travel in the air.
<i>Hakuna sababu ya kuogopa,</i>	No reason to be afraid.
<i>Ndege karibu itaondoka,</i>	The aircraft is about to take off.
<i>Hali ya hewa si nzuri,</i>	The weather is not good.
<i>Kuna mawingu na ukungu mwingi,</i>	There are clouds and much fog.
<i>Kiwanja kimetanda ukungu,</i>	The airport is covered with fog.
<i>Kuna mvua pia leo,</i>	There is rain also today.
<i>Ndege nyingi</i>	Many aircraft cannot land
<i>zinashindwa kutua shauri ya ukungu,</i>	because of fog.
<i>Karibu jua litatoka,</i>	The sun is about to come out.
<i>Ukungu umezidi siku hizi,</i>	There is too much fog nowadays.

HADITHI

Ndege moja ilikuwa angani. Rubani aliwaambia wasafiri, “Mnaweza kuvuta sigara sasa.” Baada ya muda mfupi, alitoa sauti kubwa akisema, “Zimeni sigara zenu upesi, na fungeni mikanda mara moja.” Watu wote waliogopa. Ndege ilikuwa juu ya mawingu, ikaanza kushuka upesiupesi. Chini ya mawingu kulikuwa na ukungu; rubani hakuweza kuona kiwanja cha ndege. Alijaribu kuzunguka, lakini ndege ilizidi kushuka. Mwishowe, alitua shambani. Rubani huyo alikuwa hodari sana. Japo ndege ilikuwa mbovu, lakini alitua salama, hakuna mtu aliyeumia. Ndege ilipotua, wasafiri wote walitoka wakitetemeka. Wote walimshika rubani mkono na kumpa heko kwa uhodari wake. Watu wengi walikuja kuona ajali hii ya ndege. Walishangaa walipoona wasafiri wote salama kabisa. Baada ya saa moja hivi, helikopta ilikuja ikawachukua wasafiri wote.

ZOEZI LA 45

1. Kwa nini rubani alipewa heko na wasafiri?
2. Je, ndege ilitua wapi? Kwa nini ?
3. Je, nani aliyeumia katika ndege hii?
4. Je, kwa nini watu walishangaa?
5. Je, nani alikuja kuwachukua wasafiri?

LESSON 37

KAZINI

Vocabulary

<i>kazi; kazini,</i>	work, at work
<i>kufanya kazi; kwa bidii</i>	to work with effort
<i>kufika kazini,</i>	to report for work
<i>kuchelewa kazini,</i>	to come late to work
<i>kuacha kazi,</i>	to stop working, to resign
<i>kufukuzwa kazi,</i>	to be fired
<i>lazima kila mtu afanye kazi,</i>	everybody must work
<i>mvivu wa kazi,</i>	too lazy to work
<i>hodari wa kazi,</i>	hardworking
<i>kutafuta kazi;</i>	to look for work
<i>kupata kazi,</i>	to get a job
<i>unataka kazi gani?</i>	what type of the work do you want?
<i>Kazi yoyote ile,</i>	any kind of work, no matter what kind
<i>Kulima, kupanda mbegu,</i>	to cultivate, to sow seeds
<i>Kuvuna mavuno,</i>	to harvest, harvest

Tatu ana shamba kubwa. Anafanya kazi shambani pamoja na watoto wake. Kila mwaka wanapanda mbegu nzuri za mahindi, mpunga, maharage na mihogo. Tatu hapendi mtoto mvivu. Siku moja, Mashaka alichelewa kufika shambani. Mama yake alimwambia, “Ukichelewa tena utalima peke yako wakati sisi tumekwenda nyumbani.” Toka siku ile, Mashaka hajachelewa tena kazini. Watoto wa Tatu wanajua lazima kila mtu afanye kazi. Tatu anafanya kazi kwa bidii, na watoto wake pia wanafanya kazi kwa bidii. Mwaka jana Tatu na watoto wake walipata mavuno mazuri sana. Tatu hana shida ya chakula, watoto wake kila siku wanakula chakula bora. Mara kwa mara Tatu huenda sokoni kununua samaki, vitunguu na nyama. Kila siku anawapa watoto wake chakula cha kuchukua shuleni. Jioni wakirudi, wanamsaidia kazi shambani. Mashaka ni hodari sana shuleni. Walimu wake wanampenda sana. Chausiku ameanza kusoma juzi tu. Sijali bado mdogo.

ZOEZI LA 46

1. Nani alichelewa kazini siku moja? Tatu alisema nini?
2. Tatu ana nini? Anafanya kazi na nani?
3. Nani alipata mavuno mazuri mwaka jana?
4. Je, kuna shida ya chakula kwa Tatu? Kwa nini?
5. Je, watoto wa Tatu huchukua nini waendapo shuleni?
6. Je, watoto wa Tatu hufanya nini wakirudi nyumbani?
7. Je, kwa nini Mashaka anapendwa na walimu wake?
8. Je, Sijali anakwenda shule? Kwa nini?
9. Je, Chausiku alianza shule lini?
10. Je, nani anafanya kazi kwa bidii?

Useful Expressions

<i>kumaliza kazi,</i>	to finish work
<i>kwenda kazini,</i>	to go to work
<i>kutoka kazini,</i>	to come back from work
<i>baba yuko kazini,</i>	father is at work
<i>baba hajarudi kazini,</i>	father has not yet returned from work
<i>kuanza kazi,</i>	to begin working, to start
<i>kufanya uzembe kazini,</i>	to be careless at work
<i>kuwahi kazini; kuchelewa,</i>	to be on time for work, kuchelewa
<i>kupoteza; kupoteza muda,</i>	to lose; to waste time

SHAIRI LA KUSIFU KAZI

Vocabulary

<i>Shairi,</i> poem	<i>kusifu,</i> to praise
<i>karani,</i> clerk	<i>kupanda,</i> to plant
<i>us'ende (usiende),</i> do not go	<i>adhuhuri,</i> midday
<i>ngazi,</i> step, or staircase	<i>mnazi,</i> coconut tree

(NB See also the vocabulary list at the end of this book)

1. Usende mjini kutafuta kazi ,
Utapoteza muda hiyo ni wazi ,
Kilimo shambani ndiyo hasa ngazi,

Ya maisha bora hata kiangazi,

2. Ukitaka chakula bora shambani,
Matunda, mayai , huko ni nyumbani,
Asubuhi chai , mayai kinywani,
Mchana nyama, viazi , wali jioni.
3. Utu, maisha mema, na ujirani,
Yamejenga huko bila kisirani,
Hukai peke daima asilani,
Ndugu, jirani mwaishi furahani.
4. Mjini watu hawana ujirani,
Hawajuani tarishi na karani,
Hamuna jambo wapitana njiani,
Hekaheka waenda mbio kazini.
5. Imewatawala fedha mpaka ndani,
Wakikosa hamuna raha nyumbani,
Usingizi hawapati kitandani,
Watafika mpaka huko kiwandani.
6. Nawe shika shauri kaa shambani,
Jenga nyumba yako nzuri ya thamani,
Utapata mwana umwite Shabani,
Uishi vema uwe kwako nyumbani.

(for explanation of the poem see the key)

LESSON 38

SHULE YETU

Vocabulary

<i>shule, shuleni,</i>	school, at school
<i>kusoma; kusomea,</i>	to read, to read for/to
